THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Anuani ya simu
Mkuu wa shule
0759513122

Makamu mkuu wa shule
0752141318
0758517636

Mtaaluma
0755682201

Shule ya Sekondari Kalenge,
S.L.P. 362,
KIGOMA.
29/03/2022

Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi.....
S.L.P.....
.....

YAH. **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KALENGE HALMASHAURI YA UVINZA MKOA WA KIGOMA MWAKA 2022/2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha TANO katika shule ya Sekondari **Kalenge** mwaka wa masomo 2022/2023 Tahasusi ya.....

Shule ya Sekondari KALENGE ipo umbali wa kilometa 50 mashariki mwa mji wa KIGOMA. Usafiri wa basi kutoka mjini KIGOMA unapatikana katika kituo cha mabasi STENDI YA MKOA nauli ni Tsh. 2500/= kwa watakaokuja kwa mabasi au treni kutoka mikoa ya DAR ES SALAAM, DODOMA, MWANZA, TABORA, SHINYANGA, SINGIDA, PWANI washuke kituo cha KALENGE.
Muhula wa masomo unaanza tarehe …… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni mapema, mwisho wa kuripoti ni siku 14 toka tarehe ya masomo kuanza.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 **Sare Ya shule**

(a) Sare ya shule ni rangi ya KIJANI JESHI (deep green)
Rangi ya hijabu (kijuba) ifanane na sare ya shule kwa wasichana (SKETI rinda box) na Wavulana (SURUALI).

ANGALIZO:
VITAMBAA VYA SURUALI NA SKETI (kuepuka kuchanganya rangi unashauriwa kuja kununua hukuhuku ili kuepuka changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza)

(b) Sare ya michezo kwa shule ni TRACKSUIT BLUE NA T-SHIRT YA BLUE
(d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
(e) Soksi jozi mbili NYEUSI kwa WAVULANA na NYEUPE PAMOJA NA STOCKING kwa wasichana.
(f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
(g) Sweta rangi ya KIJANI JESHI (deep green) V-SHAPE KWENYE SHINGO
(h) Nguo za kushindia (shamba dress) SURUALI NA SKETI RANGI YA KAKI NA T-SHIRT RANGI YA BLUE
(i) Tai rangi ya KIJANI JESHI
(j) T-shirt ya shule rangi ya blue bahari (light blue) yenye **nembo ya shule. (**Zinapatikana shuleni)

2.2 **Ada na Michango ya shule**

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni TSH. 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha Tsh. 35,000/=ya nusu muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.
Fedha hizo zilipwe bank kwenye **Akaunti ya shule, Namba 51601100029 NMB**, jina la akaunti ni KALENGE SEKONDARI tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip.

N.B CASH HAITAPOKELEWA SHULENI

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) Tsh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabatina samani;
(ii) Tsh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha;
(iii) Tsh. 20,000/=Kwa ajili ya taaluma
(iv) Tsh. 30,000/= Kwa ajili ya wapishi, walinzi na vibarua wengine
(v) Tsh. 2,000/= nembo ya shule
(vi) Tsh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
(vii) Tsh. 20,000/= Mitihani ya Mock kidato cha TANO
(viii) Tsh. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

ANGALIZO - Jumla ya ada na michango yote kwa mwanafunzi ni TSH. 178,000/=

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Ream ya karatasi 1 (kila muhula)
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, PURE MATHEMATICS, GEOGRAPHY, BASIC APPLIED MATHEMATICS NA GENERAL STUDIES. (Vitakaguliwa)
(iii) Dissecting kit kwa mwanafunzi wa Biolojia
(iv) Scientific calculator
(v) Godoro kwa mwanafunzi wa bweni size 2 x 6
(vi) Mashuka pair 2 blue, blanket 1, foronya (mto) 1, chandarua 1 ya bluu
(vii) Kiti na meza.
(viii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(ix) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
(x) Kwanja1, jembe 1 na mpini wake, reki 1, panga 1 na shoka 1
(xi) **Bima ya afya (NHIF/CHF). Hii ni ya lazima**.
(xii) Mifagio ya ndani wanafunzi wa
- CBG walete squizer na chelewa
- PCM walete soft bloom na chelewa
- PCB walete hard bloom na chelewa
- PGM walete toilet brush na chelewa

N.B: Vifaa vyote vinapatikana maeneo ya karibu na shule.

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu, walezi na jamii kwa ujumla;
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu, au mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
(vii) Kufunga ndevu;
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara;
(x) Uasherati,uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa;
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au kukutwa na chaja ya simu katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau bendera ya taifa;
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi (mkataba) wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai;

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule;

(d) Picha nne (4) passport size za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

(e) Pass port size mbili (2)

(f) Form four leaving certificate and result slip

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KALENGE
S.L.P.
362
KIGOMA
FOMU NAMBA 1

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi .....
2. Jina la baba.....
3. Jina la Mama.....
4. Jina kamili la mlezi.....
5. Anuani ya mzazi/mlezi.....
6. Uhusiano wa mlezi.....
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi).....
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni.....
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni.....
10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni.....
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi……..
……
.....
.....
12. Madhehebu ya dini.....
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

Jina Kamili (uhusiano)	Kazi Yake	Namba ya simu	
(a)	.....	.....	Bandika picha hapa
(b)	.....	.....	Bandika picha hapa
(c)	.....	.....	Bandika picha hapa
(d)	.....	.....	Bandika picha hapa

SHULE YA SEKONDARI KALENGE
S.L.P. 362 KIGOMA
FOMU NAMBA 2

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi.....
Jina la mzazi/mlezi.....
Anuani ya mzazi/mlezi.....
Uhusiano.....(mjomba, shangazi, kaka,dada).

Mimi.....nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi.....tarehe.....

Mimi.....
mzazi/mlezi wa mwanafunzi.....
ninaahidikuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi.....Tarehe….....

SHULE YA SEKONDARI KALENGE
S.L.P. 362
KIGOMA

FORM NUMBER 03

MEDICAL EXAMINATION FORM

To medical OfficerI/C of.....
Designated Hospital, P.O.BOX.....

Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories (a) – (m). In case of any acute or defect/ disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with specialneeds.

(a) Pupil's name.....
(b) Age.....
(c) Stool test.....
(d) Blood group .....
(e) Urine analysis.....
(f) Sphills test .....
(g) Chest test.....
(h) Speech.....
(i) Eye test …….
(j) Abdomen ……
(k) Chest X-ray.....
(l) Sickle cell test……..
(m) WCB total Differential.....

Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies .....
.....
.....
Signed by.....
Designation ……

Official Stamp
Date